

Katibu Mkuu Ikulu afungua Programu ya Mafunzo ya Uchunguzi na Mbinu za Uendeshaji Mashauri kwa Maafisa Uchunguzi na Sheria wa Sekretarieti ya Maadili.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Ikulu Bw. Peter Ilomo amefungua Programu ya Mafunzo ya Uchunguzi na Mbinu za Uendeshaji Mashauri kwa Maafisa Uchunguzi na Sheria wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanayofanyika katika Chuo cha Maafisa wa Polisi – Kidatu mkoani Morogoro.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Bw. Ilomo alisema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea Wachunguzi uwezo, kuboresha ujuzi na uelewa katika kazi ya uchunguzi na kujifunza mbinu bora zaidi na mpya za uchunguzi kulingana na mahitaji yaliyopo.

Bw. Ilomo aliendelea kusema kuwa mafunzo hayo pia yatasaidia kuboresha zaidi ujuzi wa Wanasheria katika kuendesha mashauri mbele ya Baraza la Maadili na uandaaji wa hati za mashauri.

Pia, aliwakumbusha washiriki wa Mafunzo hayo kuzingatia kuwa, Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepewa Mamlaka na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995 pamoja na marekebisho yake kutekeleza majukumu kadha wa kadha.

Bw. Ilomo aliyataja Majukumu hayo kuwa ni pamoja na kupokea Fomu za Tamko la Kiongozi wa Umma kuhusu Rasilimali, Maslahi na Madeni na Kupokea na kuyafanyia uchunguzi wa awali malalamiko kutoka kwa Wananchi dhidi ya Viongozi wa Umma yanayohusu ukiukwaji wa Masharti ya Sheria ya Maadili na kufanya uhakiki wa Tamko la Rasilimali na Madeni ya Viongozi wa Umma .

Kutokana na majukumu hayo mazito iliyopewa Sekretarieti ya Maadili, na kwa kuwa watekelezaji wakubwa wa majukumu hayo ni Wachunguzi na Wanasheria Bw. Ilomo aliwataka Washiriki wote kushiriki kikamilifu katika mafunzo hayo ili kuweza kuinua kiwango cha Utendaji kazi wao.

Akifafanua kuhusu mada zitakazofundishwa katika mafunzo hayo, Bw. Ilomo alitaja mada hizo kuwa ni pamoja na Uhakiki wa Mali na Madeni, Mbinu za kutathmini Rasilimali, Uchunguzi katika Sekta ya Umma, Utakatishaji wa Fedha, Uchambuzi na Ukaguzi wa Taarifa za Fedha na Mbinu za uendeshaji wa Mashauri na Uandaaji wa hati za Kisheria.

“Vile vile mtakuwa na nafasi ya kujifunza juu ya Maadili ya Uchunguzi na Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na.13 ya 1995 yaliyofanyika hivi karibuni. Ni wazi kwamba utaalumu wa Uchunguzi unahitajika kwani wakati mwingine itabidi kufanya uchunguzi wa mali zilizotamkwa na hata kuchunguza akaunti za benki” alifafanua Bw. Ilomo.

Naye Mkuu wa Chuo cha Maafisa wa Polisi Kidatu Kamishna Msaidizi wa Polisi Andrea Mwang'onda aliwathibitishia washiriki wa Mafunzo hayo kuwa Chuo chake kimesajiliwa na

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na mafunzo yake yamejaa vitendo zaidi na kina mazingira mazuri ya kujifunzia na kuwaasa washiriki kufuata taratibu za Chuo wakati wote watakapokuwa chuoni hapo.